03

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

# MACHI, 2024

24 Aprili 2024

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA MACHI, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA


Jumla ya matukio 125 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Machi, 2024 ambapo waathirika walikuwa 125. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 81.6, wanawake asilimia 13.6 na wanaume asilimia 4.8. Miongoni mwa watoto waathirika, wasichana walikuwa 84 (asilimia 82.4) na wavulana walikuwa 18 (asilimia 17.6).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Machi 2024**



Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 67, ambapo waathirika 60 walikuwa wasichana na saba (7) walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa nane(8) ambapo waathirika wote walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni sita (6) ambapo waathirika wawili (2) walikuwa wanawake na waathirika wanne(4) walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha ni wanne(4) ambapo waathirika watatu(3) walikuwa wasichana na mmoja(1) alikuwa mwanamke. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 11 kati ya hayo, waathirika tisa(9) walikuwa wasichana na wawili(2) walikuwa wanawake. Matukio ya shambulio yalikuwa 29 ambapo waathirika wanane(8) walikuwa wasichana, 10 walikuwa wavulana, watano (5) walikuwa wanawake na sita (6) walikuwa wanaume.


**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Machi, 2024**




Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 38) sawa na asilimia 30.4 ikifuatia wilaya ya Magharibi “B” ambapo yameripotiwa matukio 34 (asilimia 27.2).

Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, tukio moja(1) sawa na asilimia 0.8 ukilinganisha na wilaya nyengine ambapo wilaya ya Micheweni hakukuripotiwa tukio lolote kwa mwezi wa Machi 2024.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Machi, 2024**




Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 28.6 kufikia matukio 125 mwezi wa Machi, 2024 kutoka matukio 175 kwa mwezi wa Februari, 2024. Aidha, matukio yote yameripotiwa kupungua kwa mwezi wa Machi 2024.

Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 38) kwa mwezi wa Machi, 2024 ambapo wilaya ya Magharibi “B” iliripotiwa kuongoza zaidi kwa mwezi wa Februari, 2024 (matukio 43).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Februari, 2024 na Machi, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 4 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 13 | 5 | 9 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 6 | 5 | 4 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 39 | 25 | 15 | 10 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 3 | 3 | 16 | 12 |
| Magharibi 'A' | 39 | 38 | 14 | 17 | 2 | 2 | 3 | 3 | 3 | 1 | 5 | 4 | 12 | 11 |
| Magharibi 'B' | 43 | 34 | 21 | 20 | 4 | 2 | 3 | 1 | 5 | 3 | 1 | 2 | 9 | 6 |
| Wete | 8 | 6 | 6 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 4 | 4 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 2 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **175** | **125** | **84** | **67** | **11** | **8** | **6** | **6** | **14** | **4** | **23** | **11** | **37** | **29** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 19.4 na kufikia matukio 125 kwa mwezi Machi, 2024 kutoka matukio 155 yaliyoripotiwa mwezi wa Machi, 2023. Ambapo matukio yote yaliyoripotiwa mwezi wa Machi 2024 yamepungua.

Wilaya ya Magharibi “A” imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Machi, 2024 (matukio 38) ambapo wilaya ya Mjini iliongoza kwa mwezi wa Machi 2023 (matukio 43).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Machi 2023 na Machi, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 |
| Kaskazini 'A' | 6 | 4 | 5 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 5 | 1 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 7 | 6 | 4 | 4 | 2 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 43 | 25 | 19 | 10 | 8 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 3 | 12 | 12 |
| Magharibi 'A' | 34 | 38 | 14 | 17 | 8 | 2 | 1 | 3 | 0 | 1 | 4 | 4 | 7 | 11 |
| Magharibi 'B' | 36 | 34 | 17 | 20 | 5 | 2 | 2 | 1 | 2 | 3 | 1 | 2 | 9 | 6 |
| Wete | 12 | 6 | 3 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 4 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 2 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **155** | **125** | **69** | **67** | **29** | **8** | **6** | **6** | **8** | **4** | **14** | **11** | **29** | **29** |

Miongoni mwa watoto 102 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 60, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 8, Kuingilia kinyume na maumbile ni wasichana 4, Kutorosha walikuwa wasichana watatu(3), shambulio la aibu walikuwa wasichana walikuwa 9 na shambulio walikuwa 18 kati yao wasichana walikuwa 8 na wavulana walikuwa 10.

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Machi, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 5 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 20 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'A' | 30 | 16 | 2 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'B' | 30 | 18 | 2 | 1 | 3 | 0 | 2 | 0 | 2 | 2 |
| Wete | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **102** | **60** | **8** | **4** | **3** | **0** | **9** | **0** | **8** | **10** |

Miongoni mwa wanawake 17 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 7, Kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wawili (2), kutorosha alikuwa mwanamke mmoja (1), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wawili (2) na shambulio walikuwa wanawake watano (5).

**Jadweli 1.4a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Machi, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 6 | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 |
| Magharibi 'B' | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **17** | **7** | **2** | **1** | **2** | **5** |

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Machi, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Magharibi 'A' | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **6** | **0** | **0** | **0** | **6** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 52) sawa na asilimia 51.0 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 26) sawa na asilimia 25.5. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 39) sawa na asilimia 65.0 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Machi, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 2 | 0 | | | 1 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 8 |
| 6-10 | | 4 | 5 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 2 | 16 |
| 11-14 | | 15 | 2 | | | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 3 | 26 |
| 15-17 | | 39 | 1 | | | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 5 | 3 | 52 |
| **Jumla** | | **60** | **8** | | | **4** | **0** | **3** | **0** | **9** | **10** | **8** | **102** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Machi, 2024 yamepungua kwa asilimia 30.1 kufikia matukio 102 kwa mwezi wa Machi 2024 kutoka 146 kwa mwezi wa Februari 2024. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yamepungua kwa mwezi Machi, 2024 .

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Februari 2024 na Machi 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | | |
| | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Jumla Februari 2024 | Jumla Machi 2024 |
| 0-5 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 4 | 0 | 0 | 8 | 8 |
| 6-10 | 8 | 4 | 5 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 3 | 4 | 4 | 22 | 16 |
| 11-14 | 20 | 15 | 4 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1 | 4 | 1 | 8 | 6 | 40 | 26 |
| 15-17 | 47 | 39 | 1 | 1 | 1 | 2 | 8 | 1 | 8 | 1 | 11 | 8 | 76 | 52 |
| **Jumla** | **79** | **60** | **11** | **8** | **4** | **4** | **10** | **3** | **19** | **9** | **23** | **18** | **146** | **102** |


Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 23.9 kufikia matukio 102 kwa mwezi wa Machi 2024 kutoka matukio 134 kwa mwezi wa Machi 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameripotiwa kupungua kwa mwezi Machi, 2024.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Mtukio, Mwezi Machi, 2023 na Machi, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2023 | Jumla Machi 2024 |
| | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | | |
| 0-5 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 4 | 0 | 0 | 5 | 8 |
| 6-10 | 5 | 4 | 16 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 | 5 | 4 | 29 | 16 |
| 11-14 | 10 | 15 | 8 | 2 | 2 | 1 | 4 | 1 | 3 | 1 | 8 | 6 | 35 | 26 |
| 15-17 | 49 | 39 | 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 6 | 1 | 5 | 8 | 65 | 52 |
| **Jumla** | **65** | **60** | **28** | **8** | **5** | **4** | **6** | **3** | **12** | **9** | **18** | **18** | **134** | **102** |

Matukio mengi (matukio 42) yametokea Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) sawa na asilimia 33.6 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea Nyumbani kwa Mtuhumiwa (matukio 38) sawa na asilimia 30.4 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Machi, 2024**





Matukio 93 kati ya matukio 125 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 74.4 na matukio 32 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 25.6.

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Machi, 2024**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'ume | W'ke | Watoto | | | | | | | |
| | | | | Wasichana | Wavulana | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| Kubaka | 67 | | 7 | 60 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 19 | 48 |
| Kulawiti | 8 | 0 | | | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 6 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | | 2 | 4 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 |
| Kutorosha | 4 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 11 | 0 | 2 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 8 |
| Shambulio | 29 | 6 | 5 | 8 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 23 |
| **Jumla** | **125** | **6** | **17** | **84** | **18** | **0** | **0** | **0** | **0** | **32** | **93** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Machi 2024 walikuwa 125 kati yao, 102 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 81.6, 20 walikuwa jirani sawa na asilimia 16.0, wawili(2) walikuwa wapenzi sawa na asilimia 1.6 na mmoja(1) alikuwa baba mdogo sawa na asilimia 0.8.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Machi, 2024**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR MACHI 2024

Jumla ya Majalada 70 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Machi 2024, ambayo yalihusisha makosa 73.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Machi,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 7 | 8 |
| Kusini Unguja | 11 | 11 |
| Mjini Magharibi | 46 | 48 |
| Kaskazini Pemba | 5 | 5 |
| Kusini Pemba | 1 | 1 |
| **Jumla** | **70** | **73** |

Kati ya Majalada 70 yaliyopokelewa, majalada 12 yamependekezwa kufungwa, majalada 16 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 14 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 28 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 2.2: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Machi 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 7 | 1 | 0 | 0 | 6 |
| Kusini Unguja | 11 | 3 | 3 | 0 | 5 |
| Mjini Magharibi | 46 | 8 | 7 | 14 | 17 |
| Kaskazini Pemba | 5 | 2 | 1 | 2 | 0 |
| Kusini Pemba | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **70** | **14** | **12** | **16** | **28** |

Miongoni mwa makosa 73 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 39) sawa na asilimia 53.4 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Aina ya Makosa, Machi 2024**

| Mkoa | Idadi ya Makosa | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti/Kunajis | Shanbulio la Aibu/Kukashifu | Kutorosha | Uzinifu | Usumbufu wa Kingono |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 8 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini Unguja | 11 | 6 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 48 | 24 | 5 | 11 | 3 | 2 | 2 | 1 |
| Kaskazini Pemba | 5 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **73** | **39** | **7** | **14** | **5** | **4** | **3** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA MACHI 2024

Jumla ya mashauri 25 yamefunguliwa katika mahkama za Udhalilishaji kwa mwezi wa Machi, 2024 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 12) sawa na asilimia 48.0 ukilinganisha na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Machi, 2024**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika mahkama za udhalilishaji Zanzibar ni 25. Ambapo mashauri matatu (3) yametolewa uamuzi na mashauri 22 bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Machi, 2024**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Zilizotolewa uamuzi | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Faini | |
| Kubaka | 15 | 0 | 3 | 12 |
| Kulawiti | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 4 | 0 | 0 | 4 |
| Kutorosha | 3 | 0 | 0 | 3 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 1 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **25** | **0** | **3** | **22** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 25 ambapo washtakiwa wote 25 walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 14-17 (washtakiwa 8) sawa na asilimia 32.0.

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 25 ambapo waathirika watatu (3) walikuwa wanaume na waathirika 22 walikuwa ni wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 15-19 (waathirika 13) sawa na asilimia 26.3.

**Jadweli 3.2: Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Machi, 2024**


| Umri wa Mshtakiwa | Jinsi za Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Jinsi za Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 14-17 | 8 | 0 | 0-4 | 0 | 1 |
| 18-21 | 5 | 0 | 5-9 | 0 | 2 |
| 22-25 | 6 | 0 | 10-14 | 2 | 5 |
| 26-29 | 2 | 0 | 15-19 | 1 | 12 |
| 30-33 | 1 | 0 | 20-24 | 0 | 0 |
| 34-37 | 0 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 1 | 0 | 30-34 | 0 | 2 |
| 42-45 | 0 | 0 | 42-45 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 46-49 | 0 | 0 |
| 50+ | 2 | 0 | 50+ | 0 | 0 |
| **Jumla** | **25** | **0** | **Jumla** | **3** | **22** |

## WANAFUNZI NA MAHABUSU WA MAKOSA YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA WA CHUO CHA MAFUNZO

Jumla ya Wanafunzi wa makosa ya udhalilishaji waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Januari -Machi, 2024 walikuwa 35 na Mahabusu walikuwa 143.


Wilaya ya Mjini wameripotiwa kupokea wanafunzi wengi ( wanafunzi 12 ) ukilinganisha na wilaya nyengine, vilevile, mahabusu wengi wamepokelewa kutokea Wilaya ya Mjini (mahabusu 46).

**Kielelezo 4.1: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Wilaya, Januari - Machi, 2024**




Umri wa miaka 18-29 umeripotiwa kuwa na wanafunzi na mahabusu wengi zaidi ikilinganishwa na miaka mengine. Ambapo kwa upande wa wanafunzi walikuwa 23 na mahabusu ni 49.

**Kielelezo 4.2: Idadi ya Wanafunzi na Mahabusu Waliopokelewa Chuo cha Mafunzo kwa Umri, Januari – Machi 2024**



Wanafunzi wengi wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 11 na zaidi (wanafunzi 18) sawa na asilimia 51.4 ikilinganishwa na vifungo vyengine.

**Jadweli 4.3: Idadi ya Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo kwa Muda wa Vifungo na Aina ya Makosa, Januari- Machi, 2024**

| Muda wa kutumikia kifungo Chuoni (Gerezani) | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio | |
| Chini ya miezi 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Miezi 4-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Mwaka 1-2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 3 |
| Miaka 3-5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 |
| Miaka 6-10 | 1 | 1 | 6 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| Miaka 11+ | 10 | 2 | 2 | 4 | 0 | 0 | 18 |
| **Jumla** | **11** | **3** | **8** | **5** | **5** | **3** | **35** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 125 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Machi, 2024 ambapo waathirika walikuwa 125. Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 38) sawa na asilimia 30.4. Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 28.6 kufikia matukio 125 mwezi wa Machi, 2024 kutoka matukio 175 kwa mwezi wa Februari, 2024.

Matukio 93 kati ya matukio 125 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 74.4 na matukio 32 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 25.6.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Machi, 2024**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia Kinyume naMaumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 7 | [redacted] | 7 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 4 | 6 | 10 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 18 | [redacted] | 18 | [redacted] | 2 | 2 | 3 | [redacted] | 3 | 2 | 0 | 2 | 5 | 0 | 5 | 3 | 5 | 8 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 3 | [redacted] | 3 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 15 | [redacted] | 15 | [redacted] | 1 | 1 | 1 | [redacted] | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 2 | 3 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 24 | [redacted] | 24 | [redacted] | 5 | 5 | 2 | [redacted] | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 5 | 3 | 8 |
| **Jumla** | **67** | [redacted] | **67** | [redacted] | **8** | | **8** | [redacted] | **0** | **6** | **4** | **0** | **4** | **11** | **0** | **11** | **13** | **16** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Februari, 2024 na Machi, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 | Feb 2024 | Machi 2024 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 4 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 3 | 8 | 10 | 16 | 20 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 28 | 18 | 3 | 2 | 2 | 3 | 8 | 2 | 11 | 5 | 10 | 8 | 62 | 38 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 3 |
| Sehemu za kazi | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Skuli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 17 | 15 | 4 | 1 | 2 | 1 | 3 | 1 | 2 | 1 | 11 | 3 | 39 | 22 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 31 | 24 | 3 | 5 | 2 | 2 | 3 | 1 | 7 | 2 | 8 | 8 | 54 | 42 |
| **Jumla** | **84** | **67** | **11** | **8** | **6** | **6** | **14** | **4** | **24** | **11** | **37** | **29** | **176** | **125** |

Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Machi, 2024

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 25 | 10 | 0 | 0 | 0 | 3 | 12 |
| Magharibi 'A' | 38 | 17 | 2 | 3 | 1 | 4 | 11 |
| Magharibi 'B' | 34 | 20 | 2 | 1 | 3 | 2 | 6 |
| Wete | 6 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **125** | **67** | **8** | **6** | **4** | **11** | **29** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Februari, 2024 na Machi, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 | Februari 2024 | Machi 2024 |
| Kubaka | 84 | 67 | 5 | 7 | 79 | 60 | | | | |
| Kulawiti | 11 | 8 | | | | | 11 | 8 | 0 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 6 | 2 | 2 | 4 | 4 | | | | |
| Kutorosha | 14 | 4 | 4 | 1 | 10 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 23 | 11 | 5 | 2 | 19 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 37 | 29 | 7 | 5 | 11 | 8 | 12 | 10 | 7 | 6 |
| **Jumla** | **175** | **125** | **23** | **17** | **123** | **84** | **23** | **18** | **7** | **6** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Machi, 2023 na Machi, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 | Machi 2023 | Machi 2024 |
| Kubaka | 69 | 67 | 4 | 7 | 65 | 60 | | | | |
| Kulawiti | 29 | 8 | | | | | 28 | 8 | 1 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 6 | 1 | 2 | 5 | 4 | | | | |
| Kutorosha | 8 | 4 | 2 | 1 | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 14 | 11 | 2 | 2 | 11 | 9 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio | 29 | 29 | 5 | 5 | 9 | 8 | 9 | 10 | 6 | 6 |
| **Jumla** | **155** | **125** | **14** | **17** | **96** | **84** | **38** | **18** | **7** | **6** |

**Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Machi, 2024**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajis | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| 03:01 - 06:00 Mchana | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 4 |
| 06:01 - 09:00 Jioni | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| 09:01 - 12:00 Jioni | 6 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 8 |
| 12:01 - 03:00 Usiku | 31 | 2 | 2 | 2 | 4 | 6 | 47 |
| 03:01 - 06:00 Usiku | 18 | 2 | 3 | 2 | 4 | 10 | 39 |
| 06:01 - 09:00 Usiku | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 8 | 15 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 5 |
| **Jumla** | **67** | **8** | **6** | **4** | **11** | **29** | **125** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136
MMP, Zanzibar.